Chuo Kikuu chaSokoine cha Kilimo

# Jarida la HEET

*Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi*





**Ardhi ni Hazina**



**Prof. Raphael Chibunda**
*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

# Wafanyakazi SUA kunufaika na Mradi wa HEET, Pongezi kwa Rais Samia- Prof. Chibunda

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amemshukuru Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kukiwezesha chuo hicho kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi yaani (Higher Education for Economic Transformation [HEET] ambapo SUA imetekeleza adhma ya mradi huo kwa kupeleka wafanyakazi masomoni, kuongeza ujuzi, kununua vifaa vya kufundishia pamoja na Ujenzi wa Miundombinu chuoni hapo.

Prof. Chibunda alisema hayo tarehe 1 Mei, 2023 alipokuwa akizungumza na wafanyakazi katika Maadhisho ya siku ya Wafanyakazi duniani ambapo amesema Wafanyakazi wa Chuo hicho wanaendelea kunufaika moja kwa moja na fedha za Mradi wa HEET kiasi cha Sh. bilioni 73 ambazo pamoja na matumizi mengine pia zitawezesha kuboresha upande wa TEHAMA ambao Chuo hicho hakitakuwa na changamoto ya mtandao hivyo kusaidia utendaji kazi bora sambamba na ukuaji wa Teknolojia duaniani katika ufundishaji kwa njia ya mtandao.

Aidha Prof. Chibunda alipongeza namna wafanyakazi wote bila kujali vyama vyao walivyoweza kuonesha mshikamano na kushirikiana hali ambayo imechangiwa na kuwepo kwa Mwongozo mpya wa Uchaguzi wa Wafanyakazi Bora ulioanza kutumika mwaka huu na hivyo kuwataka viongozi wa vyama vya wafanyakazi vilivyopo SUA yaani RAAWU na THTU kuzichukua na kuzifanyia kazi changamoto zilizooneka katika mwongozo huo ili kuuboesha zaidi.

Akizungumzia kuhusu stahiki za wafanyakazi Makamu huyo wa Mkuu wa Chuo cha SUA alisema Serikali imetoa muongozo katika uboreshaji stahiki za wafanyakazi nchini na kwamba Chuo cha SUA kimekuwa moja ya Taasisi ambazo zimekwisha anza utekelezaji kwa wafanyakazi wake kwa kuanza kulipa madeni ya wafanyakazi , kutoa stahiki kikamilifu kwa wastaafu , kuwalipa wafanyakazi fedha za likizo kutokana na hilo ametoa agizo kwa Wakuu wote wa Idara, Ndaki, Kurugenzi na Shule Kuu kuhakikisha wanatoa ruhusa ya likizo kwa wafanyakazi kwani likizo ni haki ya kila mfanyakazi.

Pia aliwataka Viongozi kuwaruhusu wafanyakazi wote kujitokeza kushiriki katika michezo mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kushiriki mashindano ya ndani na nje ya Chuo na kuahidi kuwa kuanzia sasa SUA itashiriki shughuli za Mei Mosi ikiwemo michezo kila mwaka popote zitakapofanyika nchini.



# HEET yafadhili mafunzo kukabiliana na changamoto za magonjwa



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam) Prof. Maulid Mwatawala akizungumza wakati wa semina hiyo.*

Viongozi wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) wakiwemo Wakuu wa Idara, Ndaki na Vitengo mbalimbali wamepata fursa ya kupewa mafunzo kuhusu VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY) na Unyanyasaji wa Kijinsia mahala pa kazi lengo likiwa ni kukabiliana na changamoto mbalimbali za magonjwa zinazotokana na mfumo wa sasa wa maisha.

Akizungumza katika Semina hiyo iliyofanyika Chuoni hapo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam Prof. Maulid Mwatawala alisema mafunzo hayo yameandaliwa kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali kupitia Waraka wa Utumishi namba mbili wa 2014, kuhusu Udhibiti wa masuala hayo na kufadhiliwa na mradi wa HEET.

Prof. Mwatawala alieleza kuwa ugonjwa wa UKIMWI ni agenda kubwa ya Chuo cha SUA na umeendelea kuwa tatizo kubwa la Afya Duniani ambapo tangu kuanza kwa tatizo hilo inakadiriwa kuwa zaidi ya watu Milioni 74.6 wameshambuliwa na VVU na watu Milioni 32 wameshafariki Dunia kwa UKIMWI.

Alisema kuwa kasi ya maambukizi kwa vijana wenye umri wa miaka 15-24 ni asilimia 11.2 ambapo kundi kubwa ni la wanafunzi waliopo vyuoni na asilimia 80 wapo katika hatari ya kuambukizwa Virusi vya Ukimwi. Ameongeza kuwa ugonjwa wa UKIMWI umechangia madhara makubwa na mengi katika jamii tangu kuzuka kwake na hakuna mtu ambaye hajawahi kuguswa na tatizo hili aidha moja kwa moja au kwa mtu wake wa karibu.

Akielezea hali halisi ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza (MSY), Prof. Mwatawala alisema kuwa awali magonjwa haya yalipatikana zaidi katika nchi zilizoendelea hali iliyosababisha yaitwe magonjwa ya matajiri lakini kwa sasa imekuwa kama hali ya kawaida kutokana na kuathiri watu wa hali yoyote ile.

"Kwa mujibu wa ripoti ya WHO mwaka 2008, magonjwa sugu yasiyoambukiza yalisababisha vifo milioni 36 Duniani kote sawa na asilimia 63 ya vifo vyote ambapo kati ya vifo hivyo, asilimia 48 vilichangiwa na magonjwa ya moyo na magonjwa mengine kama vile kisukari, saratani na magonjwa sugu ya mfumo wa hewa", alieleza Prof Mwatawala.

Kwa upande wa Afya ya Akili, Prof Mwatawala alieleza kuwa kwa Tanzania pekee takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kuwa mtu mmoja kati ya wanne anakabiliwa na afya ya akili hivyo, ametoa rai kuwa wanajumuiya wa SUA wanapaswa kupewa ufahamu kuhusu magonjwa ya afya ya akili, umuhimu wa tiba na ushauri wa kisaikolojia ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

Alisisitiza kuwa takwimu hizo hazijatolewa kwa ajili ya kutisha bali ni kwa ajili ya kuonesha hali halisi ya maambukizi ili kuweza kujikinga.



# SUA yaelezea mafanikio ya Mradi wa HEET

*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Mipango, Fedha na Utawala) Prof.Amandus Muhairwa akizungumza wakati akifungua Mkutano wa Ushirikishwaji wa Wadau wa Mradi wa Mabadiliko ya Kiuchumi wa Elimu ya Juu uliofanyika chuoni hapo.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeishukuru Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuleta Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ambao umeleta tija Chuoni hapo.

Kauli hiyo ilitolewa Agosti 21, 2023 na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Utawala na Fedha SUA Prof. Amandus Muhairwa wakati akifungua Mkutano wa Ushirikishwaji wa Wadau wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi uliofanyika Chuoni hapo.

Prof. Muhairwa alisema kupitia mradi huo unaohusisha ushirikiano wa Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania, Chuo kimepata jumla ya Tsh. Bilioni 73.8 ambazo zitatumika ndani ya miaka 5 kuanzia 2021-2026 ambapo zaidi ya nusu ya fedha hizo zinatumika kwa ajili ya kuboresha upande wa taaluma na shughuli za utawala.

"Fedha hizi pia zitatumika kuongeza jengo kwa ajili ya madarasa katika Kampasi yetu ya Katavi na mabweni ikiwa ni mpango wa Sera ya Serikali kuhakikisha kila mkoa nchini unakuwa na Chuo Kikuu au Tawi la chuo kikuu litakalowawezesha wanachuo kupata elimu iliyo bora", alisema Prof. Muhairwa.

Alisema pamoja na fedha hizo kutumika kuongeza maabara ambazo zitaboresha mazingira ya kusoma na kufundishia, mpaka sasa wamefanikiwa kuwapeleka masomoni ndani na nje ya nchi walimu 41 wanaosoma Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu.

Prof. Muhairwa alieleza mafanikio makubwa ya mradi huo yatategemea ushiriki wa wanajumuiya wote wa SUA ambapo ametoa wito kwa wadau walioshiriki mkutano huo kuyaelewa.





# SUA yazindua magari Matatu kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa Mradi wa HEET



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof.Raphael Chibunda akikata utepe kuashiria uzinduzi wa magari matatu ya kurahisisha shughuli za mradi wa HEET.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) imezindua magari matatu, mawili aina ya Double Cabin na moja aina ya Land Cruiser Hardtop kwa lengo la kusaidia kurahisisha shughuli za mradi huo kwa ufanisi mkubwa ikiwemo ufuatiliaji wa masuala ya ujenzi.

Alibainisha hayo Dkt. Winfred Mbungu, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET SUA wakati akizungumza na SUAMEDIA kwenye uzinduzi wa magari hayo Kampasi ya Edward Moringe Mjini Morogoro.

Alisema wamekuwa na shughuli nyingi ambapo zingine zitaenda kuanza hivi karibuni hasa za kufuatilia mambo mengi ya ujenzi ambapo wamekuwa wakihitaji usafiri na mara nyingi wamekuwa wakitumia magari ambayo yamekuwa pia na shughuli nyingine chuoni hapo hivyo magari hayo yaliyozinduliwa yataenda kurahisisha kazi kwa sababu ni mahususi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

Dkt. Mbungu alisema wanapenda kutoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Fedha hizo walizozipata za Mradi wa HEET kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambazo zimewezesha kupelekea SUA kununua hayo magari ambapo wanatumaini yataenda kuboresha Mazingira ya watu kujifunzia pamoja na kufundishia na pia kuboresha kiwango cha wahitimu wao ambao watamaliza SUA.

"Hii ni seti mojawapo lakini tuna magari mengine tunayatarajia hapo baadae ambayo mengine yatatumika kwa mafunzo kwa vitendo zaidi kama vile mabasi pamoja na minbus kwa ajili ya kurahisisha shughuli za mafunzo kwa vitendo lakini haya tuliyoyazindua ni kwa ajili ya kufanikisha shughuli za kufuatilia utekelezaji wa Mradi amesema", Dkt. Mbungu.

Aliongeza kwa kutoa wito kwa wadau wote wakiwemo watekelezaji wa Mradi ambao ni Chuo kizima kwa ujumla kuwa washirikiane ili kuweza kutekeleza malengo ya Mradi ambao upo mahususi kwa ajili ya kuinua shughuli za kitaaluma ikiwemi Uboreshaji wa Mitaala, programu mbalimbali chuoni hapo lakini pia Miundo mbinu wezeshi ya kujifunzia na kufundishia ili ifikapo mwaka 2025/2026 kuwepo na mabadiliko yenye tija.





# SUA kuwajengea uwezo Wahadhiri kuhusu utungaji Mitaala Mtandao

Katika kuboresha ufundishaji unaoendana na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Mradi wa HEET kimeanza kutoa mafunzo kwa Wakuza Mitaala wa Chuo hicho ili kuwajengea uwezo wa uandaaji wa mitaala ya kisasa itakayoendana na wakati uliopo.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA Dkt. Jamal Jumanne alisema chini ya Mradi wa HEET unaotekelezwa hapa Chuoni wanakusudia kuwa na Mitaala ambayo itakuwa na uwezo wa kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi ikiwemo kutumia njia ya mtandao na njia ya mchanganyiko (blended).

Dkt. Jamal alieleza kuwa kupitia mitaala ambayo inaundwa, Chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili idadi kubwa ya wanafunzi ambao watakuwa na uwezo wa kujifunza katika njia rahisi ambayo itamruhusu kusoma akiwepo sehemu yoyote mbali na kukaa darasani.

"Hivyo leo tumeanza mfululizo wa Mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo Wakuza Mitaala (Curriculum Developers) wa Chuo chetu kutoka kila Idara ambapo tumeanza na Idara zilizopo chini ya Ndaki ya Kilimo Chuoni hapa na baadaye tutaenda kwa Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia na tutamalizia kwenye Kampasi yetu ya Mizengo Pinda", alisema Dkt. Jamal Jumanne ambaye pia ni Mhadhiri Chuoni hapo.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Salome Maro alisema madhumuni ya mafunzo hayo ni kuhakikisha kunakuwa na vipengele sahihi hasa katika kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao hivyo ni matumaini kuwa mafunzo hayo yatawaandaa vyema wakuza mitaala kuwa na ujuzi katika kuandaa programu zenye tija ili kukisaidia Chuo kuwa na uwezo wa kuandaa Wahitimu wenye sifa na mahitaji ya sasa.

Mmoja wa washiriki wa mkutano huo, Dkt. Gudila Anseli kutoka Idara ya Chakula, Lishe na Sayansi ya Mlaji SUA alisema Mafunzo ambayo wameyapata yatawasaidia kuongeza ujuzi wa kuandaa mitaala mizuri ambayo itawasaidia Wanafunzi wengi zaidi kujiunga na SUA kwani mifumo hiyo itakuwa na uwezo wa kumfundisha mwanafunzi hata akiwa eneo lolote.

Maboresho ya mitaala ikiwa ni sehemu ya mahitaji ya muhimu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, pindi yakikamilika yanaelezwa kuwa yatachagiza ongezeko la udahili kwa Wanafunzi wa ngazi mbalimbali Chuoni hapo pamoja na kuongeza ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji.




# SUA yasaini mkataba na Mshauri Mwelekezi wa Majengo

*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof.Raphael Chibunda (kulia) akisaini mkataba na mkandarasi aliyeshinda mkataba wa ujenzi "HABCONSULT ARCHITECT AND PLANNERS"*

Mshauri Mwelekezi wa Majengo yatakayojengwa SUA Morogoro kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) ameshauriwa kukamilisha ujenzi huo kwa wakati na ubora.

Wito huo ulitolewa na Makamu mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda wakati akizungumza kwenye hafla ya kuingia makubaliano ya kimkataba baina ya Chuo na mzabuni ambaye ni Habconsult Architect and Planners yaliyofanyika katika Kampasi ya Edward Moringe, mkoani Morogoro.


Prof. Chibunda alisema kutokana na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi kwenye taasisi nyingine za Serikali hategemei kuona ujenzi unachukua muda mrefu tofauti na makubaliano yaliyoafikiwa kwenye mkataba uliosainiwa mbele ya viongozi mbalimbali wa Chuo.

"Kwanza nikupongeze kwa kushinda hii tenda. Ni matumaini yetu kwamba pamoja na muda ambao tumekubaliana kwenye huu mkataba tungefurahi kama utaweza kukamilisha hata kabla ya muda tuliokubaliana hapa", alisema Prof. Chibunda.

Aidha, Makamu Mkuu wa Chuo alihimiza juu ya ukamilishaji wa majengo kwa ubora akisema ujenzi huo unaenda kufanyika kwa fedha za watanzania hivyo kampuni hiyo itangulize uzalendo.

Prof. Amandus Muhairwa, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa mradi huo alisema mbali na kusisitiza katika ubora wa majengo pia amemhakikishia mzabuni kuwa Chuo kitampa ushirikiano ambao atahitaji ili kurahisisha kazi jambo litakalomfanya akamilishe kwa wakati.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Habconsult Architect and Planners Bw. Nuru Habibu akiongea mara baada ya kusaini mkataba huo aliiahidi Menejimenti ya Chuo kuwa kutokana na timu ya wataalamu ambayo anayo na uzoefu wa kushika tenda mbalimbali za ujenzi wa majengo ya Serikali anaamini ataweza kukamilisha kwenye kipindi ambacho mkataba unaeleza.



# SUA ni Chuo salama kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Imeelezwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ni Chuo salama kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa ulemavu unaoonekana na usioonekana.

Hayo yalisemwa na wadau wa Elimu kutoka SUA Kampasi ya Mizengo Pinda mkoani Katavi wakati wa mafunzo ya utambuzi wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu yaliyotolewa kwa walimu , waendeshaji na wanafunzi wa Kampasi hiyo kwa ufadhili wa mradi wa HEET.

Mratibu wa Mahitaji Maalum kupitia Mradi wa HEET kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo SUA Dkt. Thabita Lupeja akifungua mafunzo hayo alisema miongoni mwa vipaumbele katika mradi wa HEET ni kuwatambua wanafunzi wa Vyuo vikuu wenye mahitaji maalum na kuwawezesha katika kuhakikisha wanafunzi hao wanatimiza malengo yao ya kielimu bila vikwazo.

"Wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa ulemavu unaooneka na usioonekana wanahitaji kuona SUA ni sehemu salama ya kuishi pamoja na kujifunza kwa kupata Elimu sawa na wanafunzi wengine na siyo kunyanyapaliwa na kutengwa", alisema Dkt. Lupeja.

Aliongeza kuwa baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo wa HEET kwa kupata fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia wamekuta kulikuwa na uhitaji mkubwa katika nyanja hiyo ya mahitaji maalumu ambapo mpaka Sasa zaidi ya wanafunzi 258 katika kampasi 2 wamegundulika kuwa wana mahitaji maalumu tofauti kwa ulemavu unaooneka na wengine usiooneka baada ya vipimo mbalimbali vinavyooambatana na mafunzo ambavyo vipimo hivyo utolewa na watalaamu wa Elimu kutoka maeneo mbalimbali wanaoshirikiana na SUA katika kutekelezaji wa mradi huu.

"Bado tunaendelea kuwabaini wanafunzi wenye mahitaji maalumu ikiwemo wenye uono hafifu, changamoto ya uziwi, kutosikia vizuri na nyingine walizozipata Sasa au awali walikuwa nazo na hawakuweka wazi ili wahitaji waweze kupata hafua stahiki katika kuhakikisha wanamaliza masomo yao wakiwa wanafunzi bora pasipo vikwazo vya kutengwa wala kunyanyapaliwa na kwenye soko la ajira kujiajiri au kuajiriwa wakawe bora", alisema Dkt. Lupeja.

Mratibu huyo alitoa wito kwa wanafunzi wanaojiunga na Chuo cha SUA kuwa wawazi ili waweze kuwezeshwa na kusaidiwa katika kuhakikisha wanajifunza vizuri na kupata huduma inayozingatia mahitaji husika ili wasome na kupata Elimu sawa na wengine.

# SUA kuanzisha Shahada mpya 32 chini ya Mradi wa HEET



Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kupitia Mradi wa HEET kinapanga kuanzisha jumla ya kozi (program) mpya za Shahada 32 ambapo timu ya Wanataaluma 32 ambao watahusika na zoezi la kukusanya maoni kuhusu Mitaala mipya ya kozi hizo imekutana kwa lengo la kujadiliana na kushirikishana ufahamu kuhusu yaliyopo kwenye dodoso litakalotumika katika kukamilisha zoezi hilo.

Akizungumza Agosti 10, 2023 Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA Dkt. Jamal Jumanne alisema Chuo kinatarajia kuanzisha Shahada za Juu 20 na Shahada za Awali 12 katika Kampasi Kuu ya Edward Moringe na Kozi 3 za Astashahada katika Kampasi ya Mizengo Pinda iliyopo Katavi.

"Kama tunavyofahamu katika zoezi hili kuna mitaala mingine itafutwa, kuna mingine itaunganishwa na kuna mitaala ambayo itapewa brand tofauti lakini pia kuna mitaala mipya ambayo itaanzishwa kwa hiyo zoezi la leo lilikuwa ni maalum kwa ajili ya mitaala ambayo Chuo kimeridhia kuanzisha", alisema Dkt. Jamal.

Akizungumzia lengo la kuwakutanisha Wanataaluma hao Dkt. Jamal alisema ni kujadili na kuwajengea uelewa kuhusu dodoso litakalotumika katika kukusanya taarifa muhimu ambazo zitakusanywa kwa njia ya Mtandao kupitia Jukwaa (Platform) ya Serikali ya Serikali Mtandao yaani e-Government Authoriy (eGA)

"Hii timu iliyokuwepo hapa ni timu itakayofanya zoezi ambalo kitalaamu tunaliita Market Survey kwenda kuuliza potential employer na potential applicants yaani wale wanaotarajia kuajiri na wale wanaotarajia kuomba kusoma kozi zetu watoe maoni yao juu ya hizi program ambazo tunazianzisha kwamba ni maarifa na ujuzi (skills) gani yaingizwe na yaboreshwe kwenye hizi program mpya", alisema Dkt. Jamal.

Nao baadhi ya Wanataaluma walioshiriki katika mafunzo hayo akiwemo Dkt. Prisila Mkenda Mhadhiri kutoka Idara ya Sayansi ya Viumbe Hai na Dkt. Nichodamus Mwasakilali Mhadhiri Idara ya Taaluma za Lugha walisema wamenufaika na zoezi hilo la kuwapitisha kwenye dodoso litakalotumika kukusanya taarifa hizo.

"Tumenufaika na zoezi hili la kutujengea uelewa wa dodoso hili la ukusanyaji wa taarifa mbalimbali na mahitaji ya hizi Shahada mpya ambazo tunazianzisha huko sokoni, sasa ili kutambua soko letu ni lipi na waajiri pamoja na wanafunzi wanaotarajia kujiunga wanataka nini, tumeelekezana, tumejadili na kuboresha dodoso hili hivyo naamini kazi itakuwa nzuri", alisema Dkt. Mwasakilali.





# Waboreshaji na Wakuza Mitaala SUA wahimizwa kuandaa mitaala mipya ya kidigitali

Waboreshaji na Wakuza Mitaala wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Mradi wa HEET wamehimizwa kuendelea na mchakato wa kuandaa mitaala mipya ya kidigitali ili kuendana na mpango ya Chuo unaoitaka mitaala hiyo kupelekwa kwa wadau wake ifikapo Oktoba 11 mwaka huu.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA Dkt. Jamal Jumanne Athuman wakati akihitimisha mfululizo wa semina za mafunzo kwa wakuza mitaala wa Kampasi ya Mizengo Pinda iliyopo Mjini Mpanda mkoani Katavi.

Dkt. Jamal alibainisha kuwa mitaala ambayo inaendelea kuboreshwa na kukuzwa na wahadhiri wa Kampasi zote tatu (Edward Moringe, Mizengo na Solomon Mahlangu) zinatakiwa zikamilike kabla ya Oktoba 10 ili kuruhusu tarehe inayofuata kupelekwa kwa wadau kwa ajili ya mapitio ya awali ya mitaala hiyo.

"Leo tumehitimisha mafunzo hapa Kampasi ya Mizengo Pinda ambapo tulikuwa na wawezeshaji wanne kila mmoja akiwasilisha kwenye eneo lake, sasa tunaanza zoezi lenyewe ambapo wakuza mitaala wanatakiwa kuhakikisha mpaka tarehe 11 ya mwezi ujao wa 10 hii mitaala iwe tayari kwa ajili ya kupelekwa kwa wadau ili ijadiliwe zaidi", alisema Dkt. Jamal ambaye pia ni Amidi wa Shule Kuu ya Elimu, SUA.



Ardhi ni Hazina




# SUA yazindua Kamati ya Ushauri wa Viwanda katika kukuza na kuinua uchumi kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia Elimu ya Juu Prof. James Mdoe (katikati, waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na Uongozi wa SUA na wafanyakazi wengine mara baada ya uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Viwanda ili kukuza na kuinua uchumi kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia - Aprili 29, 2023.*

Katika kutekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi yaani (Higher Education for Economic Transformation [HEET] project) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia Chuo Kikuu cha Sokine cha Kilimo (SUA) wamezindua Kamati ya Ushauri wa Viwanda leo Aprili 29 ili kushirikiana na Serikali katika kukuza na kuinua uchumi nchini Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Akizungumza na watekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) wakati wa Uzinduzi wa Kamati ya Ushauri wa Viwanda mgeni rasmi Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia anayeshughulikia Elimu ya Juu Prof. James Mdoe akimuwakilisha Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia alisema kuwa zoezi hilo ni moja ya utekelezaji Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020 -2025 kuufikisha mradi huo kukamilika kwa ubora na wakati ili kuboresha Elimu ya Juu.

Aidha alisema kuwa hapo awali hapakuwa na mfumo rasmi kwa Vyuo Vikuu kuwezesha kukaa pamoja na kuchakata mahitaji muhimu ili kufanikisha Elimu Bora pia ajira imepelekea kuwa na ombwe na sasa imekuwa rasmi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kama moja ya wanufaika na mradi wa HEET kamati hiyo ikasaidie kutoa wanafunzi wenye taaluma na wanaohitajika katika ulimwengu wa kazi na kufikia malengo ya viongozi wao nchini.

Naye Muwakilishi kutoka Benki ya Dunia Bw. Kaboko Mkalinga aliwataka waajiri kujitoa vyema katika utekelezaji wa mradi huo kutokana na uzoefu walionao hivyo wahakikishe wanatoa mchango wao kwa wananchi na kuhakikisha mradi huo unafanikiwa kwa kutengeneza uzalishaji wa ajira nchini.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Viwanda nchini Tanzania Bw. Akida Mnyenyelwa alisema kamati iliyochaguliwa ni muhimu kwa lengo la kuleta maendeleo ya viwanda hivyo kamati hiyo iliyoundwa ikatekeleze majukumu yake ikizingatia sekta hiyo na umuhimu wa viwanda nchini.

Aidha Bw. Mnyenyelwa alivitaka Vyuo kuwa na ushirikiano na viwanda ili waweze kujua viwanda vinavyoendeshwa ili iwasaidie kutengeneza mitaala yenye kuleta tija kwa kutambua fani na ujuzi unaohitajika kwenye viwanda pia tafiti zitakazofanywa zinazohusu viwanda kutoka SUA na Vyuo vingine nchini wahakikishe wanaleta mrejesho kwa wamiliki wa viwanda ili kutambua changamoto na wapi pa kufanyia kazi.

# SUA kuboresha Mitaala itakayozingatia mahitaji ya soko la ajira



Makamu wa Mkuu wa Chuo cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amewataka washiriki wa Mafunzo ya Kujenga Uwezo wa Kuandaa na Kuboresha Mitaala ya SUA kuyatumia mafunzo hayo kupata uelewa na kwenda kuandaa Mitaala itakayokidhi na kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

Alibainisha hayo wakati wa ufunguzi wa mafunzo hayo kwa siku ya pili ambayo ni sehemu ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) yaliyofanyika katika ukumbi wa Mabara Mtambuka Kampasi ya Edward Moringe mkoani Morogoro Aprili 25, 2023.

Prof. Chibunda alisema SUA pamoja na mambo mengine inahitaji kuboresha Mitaala yake ili kuendelea kutoa mafunzo yanayolenga kumjengea mwanafunzi ujuzi, weledi na stadi za kujiajiri na kuajirika.

Alisema ili kufikia lengo hilo SUA inahitaji mitaala inayojumuisha maarifa ya kisasa yanayolingana na mahitaji ya soko la ajira inayotilia mkazo umahiri, kukuza stadi za kazi na inayozingatia viwango vya kimataifa.

Kwa upande wake mmoja wa wawezeshaji wa mafunzo hayo Ofisa Mwandamizi wa Elimu ya Juu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya kiuchumi (HEET) ambaye ni Afisa Mwandamizi wa Elimu ya Juu Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya kiuchumi (HEET) Dkt. Evaristo Mtitu alisema kati ya mambo manne ambayo Mradi wa HEET unataka kutekeleza moja wapo ni uhuishaji na uandaaji wa Mitaala.

Alisema wanataka kuanzisha Mitaala isiyopungua 300 na kuboresha iliyopo ili ikidhi mahitaji ya sasa na baadae ya Taifa na itakayowawezesha wanafunzi kupata Maarifa au Stadi za kuajirika hivyo mafunzo haya kimsingi yataenda kuwajenea uwezo wanataaluma wa SUA katika kuhakikisha kuwa Mitaala iyoboresha inakuwa na sifa ya kumuwezesha mwanafunzi kupata ujuzi stahiki.

"Mwanzoni Mitaala ilielekeza zaidi kwenye kukuza fikra za wanafunzi lakini sio kuwawezesha kupata stadi za kuwafanya kuwa wabunifu, watafutaji au watengeneza ajira na badala yake Mitaala iliwaandaa kutegemea ajira za serikali hivyo naamini kupitia mafunzo haya wanataaluma wa SUA wataenda kwenye idara zao na kuanza kuandaa Mitaala itakayokidhi vigezo", alisema Dkt. Mtitu



**Prof. Raphael Chibunda**
Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

**Ardhi ni Hazina**




Picha za matukio mbalimbali zikionesha Timu ya Mradi wa HEET ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo pamoja na timu nyingine kutoka Taasisi za Elimu zipatazo 21 zinazotekeleza Mradi wa huo wakiwa katika mafunzo ya siku 5 ya Usimamizi wa Vihatarishi katika Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela kuanzia Desemba 4. hadi Desemba 8, 2023.









## Ardhi ni Hazina



# Kamati ya Kutathmini Ubora wa Mitaala SUA yapitia Mitaala 111

*Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA chini ya Mradi wa HEET Dkt. Jamal Jumanne akizungumza na Wanahabari (hawaonekani pichani) mara baada ya mapitio ya Mitaala 111*

Kamati iliyoundwa na Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwaajili ya Kufanya Tathmini ya Mitaala chuoni hapo imekutana kwaajili ya kutathmini Ubora wa Mitaala iliyokusanywa kutoka kwenye Idara mbalimbali za Chuo hicho ili kuipitia na kujiridhisha ubora wake kabla ya kupelekwa TCU kwaajili ya kuhakikiwa.

Aliyasema hayo Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA chini ya Mradi wa HEET Dkt. Jamal Jumanne wakati akizungumza na na Wanahabari kwenye Mkutano huo uliofanyika Ukumbi wa VETA Mikumi Mkoani Morogoro ambapo amesema walipokea Mitaala 111 na Mitaala yote imefanyiwa kazi ikiwemo iliyorudishwa moja kwa moja kuwa Idara zianze upya lakini ipo pia ambayo imepewa Maboresho.

"Napenda kuishukuru timu kwa kazi kubwa waliyoifanya kwakweli kazi haikuwa ndogo kwasababu kuna Mitaala ambayo unakuta Ina kurasa hadi 180 hivyo ni kazi kubwa lakini pia nitoe shukrani kwa Menejiment lakini pia Mradi wa HEET kwa kuwezesha hili zoezi kufanyika kwasababu tumejiridhisha sisi kama wenye Mitaala kabla ya kupeleka TCU kwaajili ya uhakiki", alisema Dkt. Jamal Jumanne.

Kwa upande wake Dkt. Nicholas Mwalukasa Mhadhiri kutoka Idara ya Infomatikia na Teknolojia ya Habari SUA alisema kazi kubwa ambayo wameifanya ni kuangalia namna ambavyo Mitaala imeandaliwa ikiwa kama imekidhi matakwa na vigezo vya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) lakini pia kuangalia kama inakidhi mahitaji ya Wahitimu kuweza kutatua changamoto hivyo wanepitia Mitaala hiyo na wanategemea baada ya hapo itaenda kuwa na ubora zaidi na kuweza kukidhi vigezo hivo.

Naye Dkt. Gaymary Bakari kutoka Ndaki ya Tiba ya Wanyama na Sayansi za Afya SUA alisema upitiaji wa Mitaala iliyokuwepo na mengine ambayo ni mipya baada ya utekelezaji wa HEET ambao umeweka mahitaji ya Mitaala kwenda na wakati lakini pia ambayo itaendana na Soko la Dunia na itakuwa wezeshi katika kujenga uwezo inafaida kubwa kwakuwa inaenda kuwawezesha wahitimu kutoka chuoni kwao kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa ubora zaidi.





# Wataalam wa Maabara SUA, wajengewa uwezo kulinda kazi za kibunifu.

*Mratibu wa Uhawilishaji na Ushauri wa Teknolojia, Dk. Doreen Ndossi akizungumza wakati wa mafunzo ya siku nne kwa Wataalam wa maabara kutoka Idara za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Mradi wa HEET kinaendelea na mafunzo ya siku nne kwa Wataalam wa maabara kutoka Idara za hapa chuoni juu ya namna ya kulinda bunifu za kazi zao ili ziweze kuleta tija kwa Chuo na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Mwandaaji wa mafunzo hayo Dkt. Doreen Ndossi akielezea kuhusu mafunzo hayo ambayo yanafanyika Kampasi ya Edward Moringe alisema ujuzi ambao wanapatiwa wataalamu wa maabara unalenga katika kuwapatia ujuzi wa namna ya kuzilinda na kuzitumia kwa usahihi tafiti na gunduzi zinazofanyika kwa manufaa ya jamii.

Dkt. Ndossi ambae pia ni Mratibu wa Uhawilishaji wa Teknolojia na Ushauri wa Kitaalam, SUA alisema wataalam hao wa Maabara wamekuwa ni watu muhimu kwenye kusaidia shughuli za kitafiti ambazo zinafanywa chuoni hapa hivyo mafunzo hayo yatawaongezea maarifa ya kujua namna ya kulinda kazi hizo ambazo wakati mwingine zinakuwa ni kazi ambazo zimefanywa na wao wenyewe.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo Mhandisi Moses Mlengera, Mkufunzi kutoka Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia, alishukuru mpango wa Chuo kutoa mafunzo hayo akisema yatawasaidia katika kuenenda sawa na maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kwa upande wake, mshiriki Veronica Rohho ambae ni Afisa Kilimo Mwandamizi kutoka Idara ya Shamba la Mafunzo 'Model Training Farm', akizungumzia manufaa ya hayo mafunzo alisema yataongeza chachu ya kujifunza zaidi kwa Wataalam wa Maabara kwa kuwa hapo mwanzo walikua wapo nyuma kwenye utafiti na ugunduzi wa mambo yahusuyo Sayansi na Teknolojia hasa kwenye upande wa Kilimo, Mifugo, na Uvuvi.

Mafunzo hayo yanaendeshwa kwa ushirikiano wa Wanataaluma kutoka SUA pamoja na Tume ya Taifa ya Sayansi COSTECH na yanatarajiwa kuhitimishwa siku ya Alhamisi Novemba 2, 2023.





# Prof. Chibunda ahimiza ushirikiano kutekeleza majukumu Kampasi ya Mizengo Pinda - Katavi

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Raphael Chibunda amewataka watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kushirikiana kiutendaji wakati wa kutimiza majukumu mbalimbali ya kiutumishi wa umma.

Prof. Chibunda ametoa wito huo kwa watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda wakati wa ziara maalum aliyoifanya katika Kampasi hiyo akiwa ameambatana na Menejimenti ya Chuo kwa ajili ya kuwaeleza watumishi hao mipango ya Chuo kwa mwaka ujao wa masomo pamoja na kusikiliza na kutatua kero za watumishi wa Kampasi hiyo.

Prof. Chibunda amewataka Watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kushirikiana katika kazi na kuendeleza utamaduni wa SUA kuwa mfano wa kuigwa kwa Jamii inayowazunguka.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa amewahimiza watumishi wa Kampasi hiyo kutosita kufika katika ofisi yoyote pindi wanapokuwa na changamoto yoyote kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi, akiwataka kuacha tabia ya kuziogopa ofisi.

Kwa Upande mwingine Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala amewakumbusha Wanataaluma kuzingatia misingi ya ufundishaji kwa kufuata Utamaduni, Utaratibu na Mwongozo wa Chuo ili SUA iendelea kuwa kitovu cha kuzalisha wanataalamu wenye tija kwa taifa.

Prof. Mwatawala ameongeza kuwa Chuo kipo katika zoezi la kuboresha mtaala wa Chuo, ambapo Kampasi ya Mizengo Pinda wamelenga kuongeza baadhi ya program ambazo zitaongeza idadi ya wanafunzi watakaosoma katika Kampasi hiyo suala ambalo litakuwa chachu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa jamii inayozunguka Chuo na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Dkt. Winfred Mbungu, Mratibu wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), akielezea maendeleo ya mradi huo kwa Kampasi ya Mizengo Pinda ambayo itanufaika na ujenzi wa majengo matatu ya kisasa, amesema Mradi huo utakamilika katika kipindi kilichokusudiwa.

Dkt. Mbungu amesema mradi huo unadhamini mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ambapo amewasihi watumishi wa Kampasi ya Mizengo Pinda kutumia fursa hiyo kujiendeleza kielimu, huku akibainisha baadhi ya watumishi waliopata udhamini wa kielimu kupitia Mradi huo.

Menejimenti ya Chuo imefanya ziara hiyo ikiwa ni mwendelezo wa kufanya ziara ya kuwatembelea watumishi wa SUA katika Kampasi, Ndaki na Shule zao, ili kuwaeleza mipango ya Chuo kuelekea mwaka ujao wa masomo pamoja na kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili watumishi hao.




# Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimeshiriki katika mkutano wa Kitaifa wa Kamati za Ushauri wa Viwanda

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilihudhuria mkutano wa IACs uliofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mkutano huo ulianza tarehe 13-16 Novemba, 2023, ukiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk Kennedy Hosea kwa niaba ya Katibu Mkuu Prof.Carolyne Nombo.

Tukio hilo lilihudhuriwa na wanachama wa IAC kutoka taasisi za elimu ya juu zinazotekeleza Mradi wa HEET. IAC inajumuisha wanachama kutoka Sekta ya Kibinafsi. Wakati wa hafla hiyo mawasilisho na majadiliano juu ya mada mbalimbali yalifanywa na kujadiliwa. Maarifa ya kutia moyo kwa ajili ya kuboresha mafunzo na wakufunzi walipewa changamoto ya kubuni na kuandaa programu na mitaala itakayokidhi mahitaji ya soko la ajira.








**Ardhi ni Hazina**

*Toleo la Pili*

# HEET



**Imetolewa na:**
Kitengo cha Mawasiliano na Masoko
S.L.P 3000, Chuo Kikuu, Morogoro, Tanzania
**Simu:** 255-023-2640006/7/8/9,
**Baruapepe:** communicationandmarketing@sua.ac.tz

**Ardhi ni Hazina**